# GRETSA UNIVERSITY - THIKA

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

## JANUARY - APRIL 2021 SEMESTER

## BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

**COURSE CODE: KISW 200**

**COURSE TITLE: FONETIKI NA FONOLOJIA YA KISWAHILI**

**DATE: 10 MAY 2021** **TIME: 8.00 AM - 11.00 AM**

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

1. SECTION A IS **COMPULSORY.**
2. SECTION B: ANSWER ANY OTHER **THREE** QUESTIONS.
3. **DO NOT** WRITE ANYTHING ON THIS QUESTION PAPER AS IT WILL BE AN EXAM IRREGULARITY.
4. ALL ROUGH WORK SHOULD BE AT THE BACK OF YOUR ANSWER BOOKLET AND CROSSED OUT.

***CAUTION:*** *All exam rooms are under CCTV surveillance during the examination period.*

**SEHEMU YA A: YA LAZIMA**

**SWALI LA KWANZA**

**a)** Ziandike sheria za kifonolojia za mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia: **[Alama 12]**
/mu + ɛrɛvu/ ------------------------------ [mwɛrɛvu]
/n + bɔvu/ ---------------------------------- [mbɔvu]
/i + a + iv + a/ ------------------------------ [[jaiva]

**b)** Ziandike sheria ulizoziandika katika (a) kwa kutumia sifa bainifu za sauti husika. **[Alama 12]**
**c)** Yaandike maneno yafuatayo kwa kutumia Alama za kifonetiki za IPA. **[Alama 10]**

- **i.** paa
- **ii.** afya
- **iii.** madhababu
- **iv.** changanya
- **v.** mvutano

**d)** Konsonanti na vokali hutofautiana kwa namna mbalimbali. Jadili. **[Alama 06]**

**SEHEMU YA B: YAJIBU MASWALI YOYOTE MATATU**

**SWALI LA PILI**

Mitazamo yote mitatu kuhusu dhana ya fonimu ina mashiko. Jadili kwa kina. **[Alama 20]**

**SWALI LA TATU**

Fafanua namna ambavyo wanaisimu wanaweza kutambua fonimu na alofoni zilizomo katika lugha ya Kiswahili. **[Alama 20]**

**SWALI LA NNE**

**a)** Taaluma za fonetiki na fonolojia zinaingiliana na kutofautiana kwa namna mbalimbali. Jadili huku ukitaja mifano. **[Alama 12]**
**b)** Lugha ya Kiswahili Sanifu haina alofoni. Yapinge au yaunge mkono madai haya. Taja mifano panapofaa. **[Alama 8]**

**SWALI LA TANO**

**a)** Ijadili michakato miwili inayotumiwa na lugha ya Kiswahili ili kupata muundo pendwa wa silabi katika maneno yake. **[Alama 10]**
**b)** Sheria za kifonolojia huwa ni muhtasari wa mabadiliko yanayokumba sauti za lugha mahususi. Fafanua kauli hii huku ukitaja mifano miwili katika Kiswahili. **[Alama 10]**